HOTUBA FUPI YA JAJI MKUU KUWAKUBALI MAWAKILI KWA NJIA YA MTANDAO TAREHE 10 JULAI 2020

- **Mhe. Jaji Mugasha, JR**
- **Mhe. Jaji Sehel, JR**
- **Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi, JK**
- **Wahe. Majaji Wafawidhi,**
- **Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu,**
- **Prof. Adelardus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**
- **Mhe. Msajili Mkuu,**
- **Mtendaji Mkuu wa Mahakama,**
- **Dr. Rugemeleza Nshala, Rais Chama cha Wanasheria Tanganyika, (TLS)**
- **Dr. Zakayo Lukumay, Kaimu Mkuu wa Shule ya Sheria,**
- **Wajumbe wa Baraza la Elimu ya Sheria (CLE): Aisha Ali Sinda; Ayubu Yusuf Mwenda; na Dr. Erasmo Nyika,**
- **Wageni Waalikwa wote,**
- **Waandishi wa Habari.**

1.1 **PONGEZI**

1.1 HONGERENI SANA MAWAKILI WAPYA. Shukrani zote siku ya leo anastahili Mwenyezi Mungu, Muumba wa mbingu na ardhi, ametupa sote ruzuku ya maisha na ambaye ametuwezesha kufikia daraja la Uwakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

1.2 Leo hii kila mmoja wenu amekamilisha safari ndefu, ni safari ya kukumbukwa iliyowafikisha katika daraja la UWAKILI.

2.0 MAFANIKIO YENU YANATOKANA NA MCHANGO KUTOKA KWA WENGINE

2.1 Mafanikio yako si matokeo ya juhudi zako wewe mwenyewe bila msaada wa watu wengine. Watu wengine wengi sana, wamechangia katika kuwafikisha katika daraja la Uwakili. Lazima mtambue uwekezaji mkubwa wa hali na mali uliofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika ELIMU kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo vikuu; ni mchango mkubwa katika mafanikio yenu. Wazazi na walezi wenu nao wametoa mchango mkubwa ambao haulipiki. Mchango mkubwa umetoka kwa ndugu zenu, marafiki, majirani, waalimu na wanafunzi wenzenu katika shule zote na vyuo mbali mbali mlivyopitia.

2.2 Rais wa zamani wa Afrika Kusini marehemu Nelson Mandela aliwahi kusema, kuwa mtu aliyefanikiwa ni yule ambaye kila anapoteleza na kuanguka, huinuka mara moja, na kuendelea na safari na kwamba, usinipime kwa kuangalia mafanikio yangu, bali hesabu mara ngapi nimeteleza, nimeanguka lakini nimeweza kuinuka na kuendelea na safari: — ***("Do not judge me by my successes, judge me by how many times I fell down***

and got up again.") Hii ina maana kuwa, pamoja na mchango kutoka kwa watu wengine, kila mmoja wenu lazima pia atambue juhudi zake binafsi, na jipongezeni kwa kustahimili changamoto zote hadi kufikia daraja la uwakili.

2.3 Siku ya furaha kama ya leo, sio siku nzuri kwa hotuba. Nitazungumza machache sana, kwa njia ya kushauriana na kubadilishana mawazo.

3.0 HAKIKISHENI KUWA KAZI ZENU ZA UWAKILI ZINALENGA "HAKI"

- Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Ibara ya 107A (1) imetamka kuwa Mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji HAKI katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama. Maneno kuwa "Kauli ya mwisho katika utoaji haki" ina maana kuwa kabla jambo halijafika Mahakamani, linapitia na kushughulikiwa na mamlaka nyingi ambazo pia, zinatakiwa zitende haki, na zikishindwa ndio Mahakama inakuwa na nafasi ya mwisho. Hivyo basi, katika kazi zenu za kila siku mnagusa haki za wananchi. Fanyeni kazi hizo kwa haki bila kusubiri mwananchi apelike shauri Mahakamani.

- NELSON MANDELA aliwahi kusema kuwa elimu ni silaha ya kuibadili dunia. Tukumbuke kuwa elimu inaweza pia kutumika

kama silaha mbaya kunyima, kudidimiza na hata kuchelewesha HAKI. Kwa umri wenu, mkijaaliwa uhai na Mwenyezi Mungu, bado mnayo miaka zaidi ya ishirini na tano mbele yenu ya kusaidia kuibadili kwa kuiboresha Tanzania kupitia taaluma yenu ya Sheria na Uwakili. Tendeni haki.

- Kazi za UWAKILI ni KAZI ya KUAMINIWA, inahitaji uaminifu binafsi wa kiwango cha juu. Unapomhudumia mwananchi, mwananchi hukuamini kwa kukupa taarifa nyingi kuhusu maswala binafsi. Ushauri wangu ni kuwa, uwakili wenu siku zote uelekezwe kwenye kuheshimu MAADILI, KATIBA, Sheria na kupatikana kwa HAKI. Siku zote kumbukeni kuwa Sheria imewapa nafasi kubwa ya kufanya mambo kwa kutegemea busara na utashi wenu. Unapotumia utashi au nafasi yako kuchelewesha uamuzi, unakuwa umekiuka malengo ya HAKI.

- Aidha, unapopokea rushwa, unakuwa umevunja malengo ya HAKI. Kwa bahati nzuri, tayari zipo Kanuni za Maadili za Mawakili za Mwaka 2018 [*Advocates (Professional Conduct and Etiquette) Regulations, 2018*] ambazo zipo kuwakumbusha Mawakili umuhimu wa kuheshimu maadili yao na kubaki katika barabara inayoelekea kwenye HAKI. Someni hizi Kanuni na zitekelezani kwa vitendo.

4.2 JITAYARISHENI KUFANYA KAZI KATIKA KARNE YA 21 YENYE USHINDANI MKUBWA:

- Katika miaka 20 ya mwanzo baada ya Uhuru wa Tanzania Bara, kila Mwanasheria aliyekuwa anamaliza masomo chuo Kikuu, alikuwa na uhakika wa kupata ajira bila ushindani wowote. Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma walikuwa na nafasi tele za ajira bila ushindani wowote. Hiyo Tanzania iliyo na ajira zisizo za ushindani haipo, na kila mmoja wenu anafahamu.

- Karne ya 21, iliyoanza tarehe 1 Januari 2001 imetajwa kuwa ni KARNE ambayo imeipa kazi ya Uwakili msukosuko mkubwa ambao taaluma ya sheria haijawahi kukumbana nao katika karne za 19 na 20.

- Mabadiliko makubwa na ya haraka ya kiuchumi, teknolojia, siasa, kijamii na hata kiutamaduni yamefanyika kwa kasi kubwa zaidi ya uwezo wa Sheria, uwezo wa Wanasheria, na uwezo wa Mawakili kuhimili mabadiliko hayo. Ili muweze kuelewa ushindani ambao kila Wakili atakayefanya kazi katika Karne ya 21 atarajie, someni **DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2025**. DIRA hii inatutahadharisha wote kuwa:

    - Karne ya 21 ni Karne yenye sifa kubwa ya ushindani katika kila kitu kinachofanyika *(The 21st Century, a century that will be characterized by competition).* Hapa, utafanikiwa kama Wakili kama utakuwa Wakili mwenye uwezo mkubwa katika sheria na uwezo mkubwa wa kushindana.

- Karne ya 21 itamilikiwa na wale wenye teknolojia ya hali ya juu *(It will be a century dominated by those with advanced technological capacity).* Wewe kama wakili, utadumu na kubaki katika ushindani wa kibiashara kama utatumia teknolojia katika shughuli zako za kiuwakili.

- Karne ya 21 itamilikiwa na kudhibitiwa na wale wenye njia bora za kuzalisha mali na kutoa huduma bora na kwa tija *(It will be a century dominated by those with high productivity).* Wakili ambaye atashindwa kutoa huduma bora, au Wakili ambaye kazi yake kubwa ni kuchelewesha usikilizwaji wa mashauri, au ambaye hatoi huduma bora—hatamudu ushindani wa karne ya 21.

- Itamilikiwa na wale wenye usafiri na mawasiliano ya kisasa *(It will be a century dominated by those with modern and efficient transport and communication infrastructure).*

- Itadhibitiwa na wale wenye ujuzi wa hali ya juu na wenye udhubutu *(It will be a century dominated by those with highly skilled manpower imbued with initiative).*
    - *Kwa kutumia lugha ya DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO, Mawakili wapya 601 nitakao wakubali leo, kumbukeni kuwa endapo mtataka kupata matunda na kushiriki katika ushindani wa karne ya*

21, ni lazima kila mmoja wenu ajiimarishe katika maeneo niliyoyataja hapo juu.

- *Kumbukeni mnaingia katika soko la ushindani ambalo tayari lina maelfu ya Mawakili waliojiimarisha.*

5.0 JITAYARISHENI KUKABILIANA NA UCHACHE WA KAZI AU AJIRA ZA UWAKILI ZILIZOZOELEKA KATIKA KARNE YA 19 NA 20:

- Siku hizi ni jambo la kawaida kabisa kwa Wanasheria waliomaliza mafunzo ya sheria kwa vitendo kutoka Shule ya Sheria na kukubaliwa kuwa Mawakili, kukosa nafasi za kuajiriwa katika Taasisi za Umma ambazo awali zilikuwa zinaajiri asilimia kubwa ya wahitimu wa shahada ya sheria.

- Changamoto hii ya Mawakili kukosa ajira rasmi inakabili pia nchi nyingi kama Australia, Marekani na Kanada ambazo zinatoa elimu ya sheria iliyo ubora wa hali ya juu lakini Mawakili hawapati nafasi katika makampuni ya Mawakili.

- Siku hizi fani zingine, na wanataalum kama Wahandisi, Wahasibu, Wachumi na kadhalika wote wanasoma Sheria na kazi nyingi za kisheria wanafanya wenyewe, bila kutafuta huduma za Mawakili.

- Siku hizi Mashirika na Taasisi za Serikali na mashirika ya Umma hawatafuti huduma za kisheria na Uwakili kutoka kwa Makampuni ya Mawakili. Siku hizi ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inafanya kazi nyingi za kiuwakili ambazo zamani zilifanywa na makampuni ya Mawakili wa kujitegemea. Kwa hiyo ajira za zamani ambazo Mawakili walikuwa wanapata hazipo tena.

- Wenzetu katika nchi zilizopata changamoto za mawakili kukosa ajira wamefanya utafiti kujua kwa nini uchumi wa nchi zao unakuwa kwa kiwango kikubwa, lakini wanasheria wao na Mawakili wanakosa ajira.

- Baadhi ya tafiti zimebaini kuwa wakati aina za ajira zinazozalishwa na maendeleo ya kiuchumi, na teknolojia; wanasheria walishindwa kutumia elimu yao ya sheria kutafuta fursa nje ya mfumo wa uwakili.

- Elimu yetu ya Sheria bado imegandishwa katika maudhui ya Karne ya 19 au 20 wakati leo hii uchumi na kasi ya dunia ipo katika karne ya 21.

- Prof Ronald J. Allen wa Northwestern University USA, alipata kuziangalia Sheria zetu za Ushahidi *(Evidence Act Cap 6)*, Kanuni ya Adhabu *(Penal Code, Cap. 16)*, Kanuni za Kuendesha Mashauri ya Jinai *(Criminal Procedure Act, Cap 20)* na Kanuni za Uendeshaji wa Mashauri ya Madai *(Civil Procedure Code, Cap*

33), akasema, Sheria hizi zimekwama kwenye mgando wa maudhui yaliyokuwa katika nchi ya India ya Karne ya 19 na zinapata shida sana kuhimili mabadiliko makubwa ya dunia inayotegemea matumizi ya teknolojia.

- Ajira ya Wanasheria, Tanzania ina picha moja ya ajabu kidogo. Mawakili wamejazana miji mikubwa na kukosa ajira, wakati maeneo mengine ya Tanzania yana upungufu mkubwa wa Mawakili.

- Chama cha Wanasheria wa Tanganyika ni vyema mkafanya utafiti ili kuweza kutathmini hawa Mawakili tunaowakubali kila mwaka, wanakwenda kufanya kazi gani? Wanafanya kazi za aina gani na wapi? Je utafiti huu unaweza kutusaidia kuwa na mitaala mipya ambayo itawawezesha Mawakili kukabiliana na changamoto za karne ya 21?

- Kutokana na kuwasaili Mawakili Wapya, nimegundua kuwa, ingawa Makampuni ya Mawakili yameongezeka katika miaka ya hivi karibuni; mawakili wengi bado wanakosa ajira za kudumu katika makampuni binafsi kutokana na ushindani mkubwa wa kugombea nafasi chache.

- Makampuni ya Mawakili mengi yamejikita zaidi katika maeneo ya mijini. Ingawa Mawakili wamesongamana katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya,

Dodoma na Tabora; maeneo mengi ya Tanzania bado hayana huduma za Mawakili.

- Baadhi ya Mawakili niliowasaili wameonyesha kutofahamu mambo mengi kuhusu maisha ya watanzania wanaoishi vijijini.

- Wengine wamejikita Zaidi katika Sheria wanazozitumia kila siku Mahakamani lakini hawafahamu mambo mengine muhimu ya kiuchumi na kimaendeleo. Kwa kutofuatilia mipango ya kitaifa tunajinyima nafasi ya kuibua fursa za kazi nje ya kazi za uwakili.

- Nawasihi Mawakili, tuielewe Tanzania na tujaribu kuibua fursa (opportunities) kutokana na miradi mikubwa- SGR, Mkongo wa Mawasiliano, Umeme Vijijini, Gesi Bwawa la kufua Umeme la Nyerere, Madini.

BIASHARA KUPITIA MIFUMO YA TEHAMA

- Nawasihi Mawakili wapya wa Tanzania tujiingize katika shughuli zingine za kiuchumi Pamoja na kufanya kazi za Uwakili. Shughuli hizi ni pamoja na kilimo, ufugaji, madini na biashara. Tuige mifano ya wanasheria wa nchi nyingine duniani ambao wamebaini kuwa Karne ya 21 inategemea BIASHARA ZA KITAIFA na BIASHARA ZA KIMATAIFA kupitia mitandao ya

TEHAMA *(ELECTRONIC COMMERCE)* na wameacha kutegemea kazi za uwakili peke yake.

- Hapa Tanzania, mawakili lazima waige mifano ya mabenki, taasisi za fedha na makampuni ya simu ambayo tayari yameshaona umuhimu wa kubadilika na wameweza kulingana na matakwa ya ushindani wa kibiashara wa karne ya 21 kwa kufanya biashara na mihamala yao kupitia mitandao kwa saa ishirini na nne (24).

- Sheria za Tanzania tayari zimeweka mazingira ya kufanya biashara kwa njia ya mitandao. Mifano hapa ni pamoja na— SHERIA YA MIHAMALA YA KI-ELEKTRONIKI YA MWAKA 2015 (**ELECTRONIC TRANSACTIONS ACT, 2015)**, SHERIA YA MAKOSA YA MITANDAO (**CYBER CRIME ACT, 2015)**, Sheria iliyounda Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mabadiliko katika Sheria ya Ushahidi, Usajili wa Raia na wasio raia, Paspoti mpya za kielektroniki, usajili laini za simu kwa njia ya biometriki na hata anuani za Makazi (**post code**). TEHAMA tayari imetungiwa kifungu maalum cha sheria ili itumike na Polisi kurekodi mahojiano na watuhumiwa kwa njia ya sauti na kwa njia ya VIDEO.

- Kifungu cha 57(5) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ilifanyiwa mabadiliko na Sheria Namba 7 ya 2018, kwamba, badala ya polisi kuandika maelezo ya watuhumiwa

kwa mkono na kuzua mabishano baadaye mahakamani, sasa hivi polisi wanaweza kurekodi sauti na picha za video za mahojiano. Hii inalenga kuweka uwazi katika shughuli za upelelezi na ukusanyaji wa Ushahidi na kupunguza uwezekano wa watuhumiwa kuandikisha maelezo kwa hiyari lakini baadaye kubadilika. Aidha hupunguza malalamiko ya watuhumiwa kuwa walilazimishwa kuandika maelezo au walibambikiwa kesi.

- Sheria na taratibu hizi za TEHAMA, ni vipande vipande vya mabadiliko makubwa ambayo ukiviunganisha unapata mazingira ya Mawakili Pamoja na watanzania wengine kushiriki katika shughuli za kibiashara kupitia mitandao.

4.3 MATUMIZI YA TEHAMA HAYAKWEPEKI

- Katika miaka michache ijayo, wakili ambaye hatakuwa na uwezo wa kutumia TEHAMA atapata wakati mgumu sana kufanya kazi za Uwakili katika Mahakama za Tanzania. Muda si mrefu, mashauri yote yatatakiwa kusajiliwa na kuwasilishwa Mahakamani kwa njia ya mtandao na tayari kanuni za kusajili mashauri ya madai *(Electronic Filing Rules)* zinatumika.

- Mahakama tayari inao Mfumo ya kielekitroniki wa kusajili na kuratibu mashauri (JSDS2) ambao tayari unafanyakazi tangu 6 Februari 2019. Mfumo huu wa JSDS2 unawezesha kufanyika kwa urahisi kwa mambo

mbalimbali ya usimamizi wa Mashauri kama—kufungua shauri kielekitroniki, na hata kuitwa shaurini/kupata taarifa za shauri kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu – *(sms notification)*.

- Wengi wenu ni watumiaji mahiri wa TEHAMA kwa hiyo mtakuwa sambamba na matumizi ya TEHAMA katika shughuli za utoaji haki.

- Ninaamini upungufu wa ajira kwa Mawakili wapya utapungua kadri matumizi ya TEHAMA katika shughuli za kimahakama na za kibiashara zitakapokuwa zikiongezeka. Karne ya 21 itatawaliwa na biashara kupitia mitandao *(commercial transactions conducted electronically on the Internet)* itahitaji Mawakili wenye uwezo mkubwa katika TEHAMA ambao ni nyinyi Mawakili wapya.

- Janga la COVID-19 lililazimu Mahakama ya Tanzania kutumia TEHAMA kuhakikisha kuwa shughuli za utoaji haki zinaendelea. Huu ni mfano mzuri wa faida ya TEHAMA.

- Hadi kufikia tarehe 8 Julai 2020 jumla ya mashauri **3874** yalipokelewa kupitia mitandao ya Mahakama.

- Mafanikio makubwa yameonekana kwa usikilizwaji kwa njia ya *video conference*, ya mashauri ya wadaawa walioko Magerezani:
    - Katika kipindi cha tahadhari ya COVID-19 magereza yote yalikuwa katika ZUIO (LOCK-DOWNS). Hata hivyo, mashauri ya jinai na rufani za jinai ambazo ziliwahusu wafungwa na mahabusu, zimeendelewa kusikilizwa kwa njia ya Tehama *(video conferencing)*. Hadi kufikia tarehe 8 Julai 2020, jumla ya mashauri **8,815** yamesikilizwa katika ngazi ya mahakama mbalimbali kwa njia ya TEHAMA.

    - Mafanikio haya yamewezekana baada ya Mahakama ya Tanzania kununua vifaa vya TEHAMA na kuvisambaza kwenye Magereza **16**. Vifaa vya TEHAMA ni Pamoja na SMART TV thelathini **(30),** Kamera thelathini **(30)**, LAPTOPS thelathini **(30)** na viunganishi vya sauti na picha za video (HDMI) thelathini **(30)**. Jumla ya Gharama ya Vifaa ni Tshs. **230,018,661.40/-**.

    - Vifaa hivi vimesambazwa katika magereza ya **Ukonga**, **Segerea**, **Mwanza**, **Tabora**, **Mtwara**, **Mbeya**, **Tanga**, **Musoma**, **Arusha**, **Moshi**, **Dodoma**, **Sumbawanga**, **Shinyanga**, **Iringa**, **Bukoba** na **Songea**.

- Kadri ya usambazaji wa umeme unavyoendelea vijijini, hivyo hivyo ndivyo huduma za Mahakama Mtandao zitakavyokuwa zikifikishwa katika sehemu mbali mbali za nchi yetu. Ni matumani yangu kuwa huduma zenu za Uwakili zitasogea hivyo hivyo, kadiri TEHAMA inavyotumiwa na Mahakama ya Tanzania.

- Mawakili wapya lazima mtambue kuwa Mahakama inapotumia TEHAMA, wadau wa Mahakam ana mawakili wote ambao ni Maafisa wa Mahakama; lazima nao wahakikishe kuwa wanatumia mifumo ya TEHAMA.

- Hakikisheni kuwa ofisi za Wakili mtakazofungua zinakuwa na vifaa vya kisasa vya kuwawezesha kukutana na wateja wenu bila ya hao wateja kufika ofisini kwenu. Huo ndio uwakili wa karne ya 21.

5.0 KARNE YA 21 NI YA KUJIENDELEZA, KUJISOMEA NA KUJIONGEZEA UWEZO WA ZIADA NJE YA TAALUMA YA SHERIA

- Hakuna Chuo au Taasisi yoyote ya elimu ya Sheria itakayoweza kuwapa elimu ambayo itakidhi kila badiliko linalojitokeza duniani. Kujisomea na kujiendeleza ndio chuo chako kikuu.

- Kwa mujibu wa ripoti ya JUKWAA LA UCHUMI DUNIANI (World Ecoomic Forum) la Januari 2016, ilibashiri kuwa katika kipindi cha miaka mitano baada ya 2016 zaidi ya asilimia 35 ya utaalamu na ujuzi mbalimbali uliokuwepo mwaka 2016 na ambao ulichukuliwa kuwa ni muhimu mwaka huo wa 2016 utabadilika.

- Hii ina maana kuwa Taaluma ya Uwakili tuliyo nayo leo, inaweza isitoshe kutatua changamoto mpya zitakazojitokeza baada ya miaka mitano ijayo. Kila siku WAKILI hana budi kujisomea na kujifunza mambo mapya yanayojitokeza kila siku!

- Kamati ya Chama cha Mawakili wa Jimbo la Australia ya Magharibi ilishauri kuwa, katika kukabiliana na USUMBUFU/MABADILIKO/CHANGAMOTO, Mawakili wajisomee ili wajiongezee ELIMU, UJUZI na MAARIFA katika maeneo yaliyo nje taaluma ya Sheria. Elimu ya Sheria Endelevu (Continous legal education) inayotolewa na TLS, ni mfano mizuri.

- Karne ya 21 inahitaji Mawakili wenye ufahamu na ujuzi mkubwa wa Sheria, lakini wawe pia na ziada ya uelewa na ujuzi katika Sheria za Kimataifa, Sheria za Kikanda na pia wawe ni wenye uwezo mkubwa wa kushirikiana na kufanya kazi pamoja na wanataaluma wa fani nyingine kama **Wahandisi**, **Wahasibu**, **Madaktari**, na kadhalika.

- Ningependa kuchukua nafasi hii kuliomba BARAZA LA ELIMU YA SHERIA TANZANIA (CLE), kwa kushirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Vitivo vya Sheria vya Vyuo Vikuu, Pamoja na Shule ya Sheria kwa Vitendo (Law School of Tanzania), na Chama Cha Mawakili wa Tanganyika (TLS)— tufanye tathmini, Je elimu ya Sheria tunayoitoa inakidhi ushindani wa Karne ya 21? Wenzetu katika nchi zilizoendelea tayari wameanza kubadili mitaala, hatuna budi kufanya hivyo haraka.

Mwisho

- Mimi nina imani kuwa elimu na taaluma ya Sheria mliyopata itawawezesha kushindana katika Karne ya 21. Kama mtajisomea kujiendeleza na kukubali kuwa Taaluma ya Sheria bila ushirikiano na taaluma zingine haiwezi kufanikiwa.

- Ni matumini yetu kuwa mtatumia UWAKILI WENU kwa faida na manufaa ya TANZANIA.

MUNGU AWABARIKI, ASANTENI KWA KUNISIKILIZA